# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS IKULU KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

Mheshimiwa Spika, kila sifa njema anastahiki Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia Uzima na Afya njema ambavyo vimetuwezesha kukutana tena katika Baraza hili kwa lengo la kujadili na kuidhinisha Mapato na Matumizi ya Fedha za Serikali yetu Tukufu. Vile vile, nachukua fursa hii kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika pamoja na wasaidizi wako kwa kuliongoza vyema Baraza hili Tukufu kwa umahiri mkubwa na ninaamini kwamba mtaendelea kuliongoza kwa uadilifu wa hali ya juu.

Mheshimiwa Spika, napenda pia, kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa uamuzi wake wa kuirejesha tena Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, hatua ambayo inaongeza hadhi na heshima kwa nchi yetu. Kamati inaridhia sana juhudi za Mheshimiwa Rais za kutembelea maeneo mbalimbali ya nchi yetu na kutatua matatizo ya wananchi. Aidha, uadilifu anaotuonesha unapelekea kupatikana kwa maendeleo pamoja na kudumu kwa amani na utulivu wa Taifa hili.
Tunamuomba Mwenyez Mungu azidi kumpa hekma busara na nguvu katika utumishi

wake.

**Mheshimiwa Spika,** pia, sina budi kumshukuru Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Ikulu Mheshimiwa Jamal Kassim Ali kwa umahiri wake uliomfanya aweze kuteuliwa tena kuwa Waziri katika Wizara hii mpya pamoja na kuwapongeza watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu pamoja na Naibu Katibu Mkuu kwa mashirikiano yao waliyotupatia wakati wa kupitia makadirio ya mapato na matumizi ya Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, nachukua fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisishia kazi yangu ya kuongoza kikao kuwa nyepesi zaidi, kwa hakika ni Wajumbe mahiri sana. Pia, wameweza kuijadili ipasavyo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha kwa Wizara hii zinatumiwa kwa matumizi yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima ya hali ya juu kabisa napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama ifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| *1.* | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| *2.* | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| *3.* | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| *4.* | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| *5.* | Mhe. Zaina Abdulla Salum | Mjumbe |
| *6.* | Mhe. Mohamed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| *7.* | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| *8.* | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| *9.* | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Ikulu imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984, kifungu cha 50(4). Na kuanza utekelezaji wake tarehe 10/07/2021. Ofisi hii katika kusimamia na kutekeleza Bajeti yake, ina jumla ya Mafungu *mawili (2)*

ambayo ni **Fungu** *A 01* – Afisi ya Rais  Ikulu na **Fungu** *A 02* – Baraza la Mapinduzi.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara hii ina jumla ya Programu kuu *sita (6)* ambazo ni:

*(i)* Kusimamia na Kuratibu Shughuli na Huduma za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu;

*(ii)* Kuratibu Ushirikiano wa kikanda, Kimataifa na Wazanzibari Wanaoishi Nje ya Nchi;

*(iii)* Utawala na uendeshaji wa Afisi ya Rais Ikulu;

*(iv)* Uimarishaji wa kumbukumbu na nyaraka;

*(v)* Uratibu wa Majukumu ya kikatiba na kisheria ya Baraza la Mapinduzi; na

*(vi)* Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza la Mapinduzi.

## FUNGU *A 01* – AFISI YA RAIS IKULU

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu imeridhishwa na vipaumbele vya **Fungu A 01** lenye kuonesha uimarishaji wa Mazingira na usalama katika nyumba za Ikulu Unguja, Pemba, Dar es Salaam na Dodoma. Kamati imefarijika na mpango wa kuzifanyia matengenezo nyumba za viongozi na pia kujenga "state lodge" mbili.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati katika kipindi kilichopita ilifanikiwa kuitembelea Ikulu ndogo ya Micheweni, Kisiwani Pemba; Ikulu ambayo anaitumia Mheshimiwa Makamo wa Kwanza wa Rais wakati wa ziara zake za Kisiwani Pemba. Kamati haikufurahishwa na hali ya Mazingira iliyokutana nayo katika makaazi hayo. Hivyo, Kamati yangu inashauri kufanyiwa ukarabati wa nyumba zote na ofisi zilizomo katika eneo hili kwa kuwa Bajeti yake tayari imeshaombwa kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, kupitia Kifungu **PA0101** cha programu ya Kusimamia na Kuratibu Shughuli na Huduma za Mheshimiwa Rais na Kuimarisha Mawasiliano Ikulu, Kamati inashauri kuongeza Mawasiliano katika maeneo ya vijijini ili huduma ya *Sema na Rais* iweze kuwafikia wananchi waliowengi katika maeneo hayo kwa kuwa watu wote wanahaki sawa ya kutoa maoni yao.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uratibu wa shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kikanda na Kimataifa, Kamati inasikitishwa na uchache wa fedha walioyopatiwa kwa kipindi hiki, jambo ambalo linapelekea Serikali kuwa na ushiriki mdogo wa mikutano na makongamano mbali mbali ya kikanda na kimataifa kutokana na ukosefu wa fedha. Hata hivyo, Kamati inashauri fedha zinazoidhinishwa kutumika kupitia Bajeti ya Ofisi hii, kuingizwa kwa wakati na kwa kiwango kilichopangwa ili kuweza kusimamia programu hii na kukamilisha malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa programu kuu ya *PA 0104 Uimarishaji wa Kumbukumbu na Nyaraka* ambayo inasimamia Taasisi ya Nyaraka yenye jukumu la kutunza nyaraka na kuhifadhi kumbukumbu zote za Taasisi na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania kwa zile Taasisi zilizopo Zanzibar. Kamati haikuridhishwa na kiwango cha fedha walichopangiwa kukusanya cha Tzs.15,000,000/- kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Kupitia *Kasma A0112*, fedha hizi ni nyingi kutegemea na vyanzo vyao ambapo kwa kiasi kikubwa wanategemea mashine ya fotokopi kwa ajili ya wageni wanaotembelea hapo kwa shughuli za kiutafiti, licha ya makusanyo ya ada za utafiti kupelekwa Taasisi nyengine tofauti na hii. Sambamba na hilo, Kamati inasisitiza kuboreshwa kwa vifaa vya Taasisi ya Nyaraka na kuhakikisha vinakua bora na imara katika kurahisisha utendaji wa kazi zao.

FUNGU *A 02* – BARAZA LA MAPINDUZI

Mheshimiwa Spika; Kwa upande wa Baraza la Mapinduzi, Kamati inatoa pongezi zake za dhati kwa namna wanavyosimamia majukumu yao na kuhakikisha kwamba Serikali yetu imara imefanikiwa katika usimamizi na utekelezaji wa maagizo yake kwa mujibu wa Katiba ya nchi. Aidha, katika kuona shughuli za utumishi na uendeshaji za Baraza la Mapinduzi kupitia programu ya *PA 0202 Utumishi na Uendeshaji wa Ofisi ya Rais Baraza la Mapinduzi,* Kamati inashauri fedha zilizopangwa kwa ajili ya "*Matumizi ya*

*Uendeshaji wa Ofisi"* kuingizwa kwa wakati na kwa kiwango cha kuridhisha kwani kwa mwaka huu wa 2022/2023 ofisi hii imeingiziwa wastani wa aslimia 53% ya fedha zilizopangwa kutumika. Aidha Kamati inaiomba Ofisi kuliangalia suala la maslahi ya watumishi wake kwa umakini zaidi kutokana na unyeti wa ofisi hiyo, majukumu yao ya usimamizi wa kazi na majukumu yao makubwa wanayotekeleza katika Serikali yetu.

*HITIMISHO*

**Mheshimiwa Spika,** shukrani za pekee naomba ziende kwa Raisi wetu mpendwa Mheshimiwa, Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa namna alivyoileta miradi ya UVIKO 19 ambayo itawasaidia sana wananchi wetu kujikwamua kiuchumi na kijamii. Ushauri wetu ni kuwaomba waheshimiwa wajumbe wa Baraza lako Tukufu kuisimamia kikamilifu miradi hii na kuhakikisha tunaiunga mkono katika utekelezaji wake kwa lengo la kutimiza azma ya Serikali yetu katika kuwatumikia wananchi wake.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho, napenda kuchukuwa fursa hii kukushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha maoni machache sana ya Kamati yangu, kwa niaba ya Kamati pamoja na kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako kwa kunisikiliza kwa umakini wakati wote wa uwasilishaji wa maoni yetu.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho kabisa, nihitimishe kwa kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waichangie, wairidhie Bajeti hii na hatimae waiidhinishie Ofisi ya Rais Ikulu, Makadirio ya Mapato na Matumizi Fedha zilizopangwa kutumiwa katika mwaka wa fedha *2022/2023* ili wapate kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ***Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

Ahsante,

…………………………….

(Machano Othman Said)

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,**

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR